**Consolata Missionaries**

**Roma**



# NOVENA
# YA
# MT. JOSEPH ALLAMANO



**ROMA**

# NOVENA YA MT. JOSEPH ALLAMANO

## Mwanafamilia, aliyeanzisha Familia ya Wamisionari, ili kuufanya ulimwengu kuwa Familia Moja ya Mungu



### Siku ya 1 - Allamano na baba yake, Joseph Allamano

**Kwa jina la Baba...**
**Wimbo wa Mt. Allamano**

**Kiongozi:**

Mwenyeheri Allamano alizaliwa huko Castelnuovo D'Asti - leo Castelnuovo Don Bosco - kutoka kwa Joseph Allamano na Marianna Cafasso. Alikuwa mtoto wa nne kati ya watoto watano. Hakuna habari nyingi kuhusu babake Allamano, lakini tunajua kwamba alikuwa na kaka ambaye alikuwa kasisi (Padre John Allamano) na alikufa tarehe 2 Desemba 1853, wakati Mtakatifu Allamano hakuwa bado na umri wa miaka mitatu.

Kulingana na mpwa wake alikuwa Mkristo mzuri. Wazazi wote wawili wa Mt. Allamano walikuwa wakiishi kijijini; walikuwa Wakristo bora na wafadhili wema wa wahitaji. Baba yake Mt. Allamano alikuwa mtu mwaminifu sana kwa mke wake na pia alikuwa mcha Mungu. Kama wengi katika kipindi hicho, hakujua kusoma na kuandika, lakini imani na hekima yake ilipita masomo ya darasani.


Baba yetu ....
Salamu Maria...



**SALA**: Tunakushukuru, Bwana, kwa kulipatia Kanisa lako Mt. Joseph Allamano. Ulimfanya kuwa shahidi wa upendo wako, mwalimu wa mapadre na baba wa wamisionari kwa ajili ya uinjilishaji wa watu wote. Utujalie, Bwana, tunachoomba kwa maombezi ya huyu mtumishi wako mwaminifu, msimamizi wa Faraja ya Maria duniani. Mfano wake na utupatie changamoto ya kukutafuta wewe juu ya yote na kufanya kazi kwa manufaa ya wote. Amina.



## Siku ya 9 - Allamano na msaada wake kutoka Mbinguni



**Kwa jina la Baba...**

**Wimbo wa Mt. Allamano**

Mnamo tarehe 16 Februari 1926, 4:10 asubuhi huko Italia, Padre Joseph Allamano alirudi kwa muumbaji wake.

"Nimeishi miaka yangu mingi kwa ajili yenu; Nimetoa mali yangu, afya yangu na maisha yangu kwa ajili yenu; Natumaini kwamba baada ya kifo changu, nitakuwa mlinzi wenu mbinguni" aliandika padre Allamano katika Wosia wake kwa wamisionari wake. Kutoka Mbinguni aliahidi kufanya zaidi kuliko vile alifanya hapa duniani." Kutoka Mbinguni, anaendelea kuwa… baba yetu!

Maombezi yake kwa ajili ya wamisionari wake, maombezi yake kwa ajili ya kazi ya kimisionari kwa ujumla, maombezi yake kwa watu wengi ambao duniani kote wanamwita kupokea neema za pekee kutoka kwa Mungu ni ushuhuda wa mtu ambaye bado yu hai kikamilifu katika ushirika wa Watakatifu.

Tunaposhukuru Mungu kwa ajili ya kutangazwa kwake kuwa mtakatifu, tunaomba kwanza kabisa roho ya kimisionari iendelee kukua ndani yetu, katika familia ya Wamisionari wa Consolata ya Mapadre, Mabruda, Masista na Walei na katika dunia nzima.

Baba yetu ....
Salamu Maria...

**SOMO: Mathayo 25: 31-46** **(Wazo kuu: Siku ya mwisho kipimo cha maisha yetu kitakuwa Upendo.)**

*(Baada ya tafakari fupi)*
Atukuzwe Baba na Mwana...



**SOMO: Yohane 17:1-22** **(Wazo kuu: Uhusiano wa Yesu na Baba – Uhusiano wetu na Mungu)**

*(Baada ya tafakari fupi)*
Atukuzwe Baba na Mwana...

**Kiongozi:**

**SALA**: Mt. Joseph Allamano, ulijua maana ya kuwa na wazazi wahisani na jinsi walivyofundisha moyo wako kuwa wazi kwa mahitaji ya ulimwengu. Ulijua pia uchungu wa kutokuwa na baba yako tangu ujana wako. Utuombee sisi na hasa wale waliofiwa na baba zao na bado wanateseka na maumivu yake. Tunaomba waweze kusonga mbele katika maisha yao kwa kuungwa mkono na wanafamilia wengine. Utuombee tuwathamini baba zetu kwa jinsi walivyo na sio elimu ya kiakili waliyo nayo au kwa nafasi yoyote wanayoipata katika jamii. Tunaomba kwamba akina baba wote wazitunze familia zao wakifahamu kwamba wameitwa kuwa sura ya Mungu Baba na Kristo mwenyewe. Maria Consolata, utuombee! Mtakatifu Joseph, mfanyakazi utuombee! Mt. Joseph Allamano, utuombee!



## Siku ya 2 - Allamano na mama yake, Marianna Cafasso



**Kwa jina la Baba...**
**Wimbo wa Mt. Allamano**

Mama wa Mt. Joseph Allamano alikuwa Marianna Cafasso, dada wa Mtakatifu Joseph Cafasso. Tunasoma kwamba alikuwa mwanamke mwenye maadili ya hali ya juu na mama wa mfano. Alijitolea kikamilifu kwa elimu ya watoto wake, hisani kwa mtu yeyote anayeteseka na aina yoyote ya maumivu na huzuni, alikuwa mkarimu na tayari kila wakati kwa faida ya wengine. Alikuwa mkarimu sana - nyumbani kwake kulikuwa na nafasi kwa kila mtu. Mt. Allamano anatambua elimu ya maadili na dini aliyopokea kutoka kwake. Alikuwa akiwasomesha watoto si kwa ukali bali kwa usahihi. Ndani ya nyumba kulikuwa na utaratibu mwingi. Mt. Allamano anahusishwa na mapenzi nyororo ya mama yake; alikuwa haondoki nyumbani mara nyingi, ili kuendelea kuwa karibu na mama yake.

Alikuwa akimtaja mama yake kama "Yule mwanamke mtakatifu… mama yangu". Mmoja wa wapwa wake aliandika: "Walipokuwa watoto wadogo wakifanya makosa ambayo alikuja kujua, wao, badala ya kukimbia kwa hofu ya kuadhibiwa, walikuwa wakienda kupiga magoti mbele yake, baada ya kutambua kosa lao. Walikuwa wakisikiliza kwa heshima maoni yake na walikuwa tayari kujirekebisha". Alikubaliana na maamuzi ya Mt. Allamano kuhusu masomo yake. Allamano alikuwa mtu mwenye utulivu sana, asiye na heka heka, shida au mashaka.

Hata kama alikuwa na maisha ya utulivu, kwa namna fulani alikuwa na huzuni. Hii ni kwa sababu ya mama yake aliyekuwa mgonjwa na pia kutokana vifo vingine katika familia yao. Yeye mwenyewe alisema kwamba mara nyingi sana alitumia likizo yake



Baba yetu ....
Salamu Maria...

**SOMO: Luka: 24:1-11** **(Wazo kuu: Wanawake ni mashahidi wa ufufuko. Wanafaa kushirikishwa kazi za kuinjilisha pia).**

*(Baada ya tafakari fupi)*
Atukuzwe Baba na Mwana...

**SALA**: Mt. Joseph Allamano, ulijua jinsi ya kuwa karibu na familia yako na familia zako mpya za kiroho na za kimisionari. Kila mtu hakuwa msaidizi tu au mfanyakazi, lakini wote walikuwa mama yako, kaka yako na dada yako. Utuombee ili tuweze kutengeneza uhusiano wa kifamilia na wale tunaoishi nao, wale tunaofanya nao kazi na wale tunaohusiana nao. Maria Consolata, utuombee! Mtakatifu Joseph, mfanyakazi utuombee! Mt. Joseph Allamano, utuombee!



## Siku ya 8 - Allamano na Masista Wamisionari wa Consolata



**Kwa jina la Baba...**
**Wimbo wa Mt. Allamano**

Baada ya kuwa na Masista wa Cottolengo wakisaidia katika misioni nchini Kenya, Mt. Joseph Allamano alitambua kwamba misioni ilihitaji masista wamisionari kamili. Kwa maneno mengine, sio tu akina dada walio tayari kwenda kusaidia katika misioni bali akina dada ambao wana wito kamili wa umisionari.

Baada ya muda wa sala na utambuzi (tafakari), Mt. Allamano alianzisha Masista Wamisionari wa Consolata tarehe 29 Januari 2010. Alizungumza na kundi la kwanza lililoondoka kwenda Kenya kwa maneno haya: "Zaidi ya yote, kumbukeni kwamba mna lengo moja tu, kuwa watakatifu na kuokoa roho nyingine nyingi pamoja nanyi. Kwa kufanya hivyo, mtakuwa mnaishi kulingana na wito wenu mkuu, na mtapata tuzo kubwa Peponi.

Zaidi ya yote, mnapaswa kuwa na roho ya imani, utii, upendo na ya kujitakasa...Ninapendekeza hasa upendo wa kindugu. Pendaneni kama akina dada katika Bwana wetu Yesu Kristo, saidianeni katika mapungufu yenu, pendaneni na kurekebishana.... Ninakusalimu kwa upendo wa kibaba, nikiwahakikishia sala zangu asubuhi na jioni kila siku kwa ajili yenu katika altare ya Mama yetu Consolata.

Mt. Allamano alikuwa anakwenda kila siku kwa jumuiya ya Masista wa Consolata kuwatembelea na kuwashirikisha kuhusu maisha ya kiroho na kuwatia moyo katika maisha yao yaliyowekwa wakfu kwa ajili ya utume. Wangemwita "baba" – ishara ya uaminifu na uhusiano mwema uliokuwa umeundwa kati yao wenyewe.



kuketi karibu na mama yake mgonjwa, ambaye alikuwa akihamishwa kutoka kitanda hadi kwenye na kutoka kwenye kiti hadi kitanda. Mama yake alipokuwa bado ana uwezo wa kusikia, kijana Joseph alimsomea vitabu, jambo ambalo angependa sana... Ilimbidi amwambie wakati mwingine: "Nenda nje ukapumue hewa kidogo..." Kila mara Mt. Allamano aliondoka nyumbani kwenda seminari, mama yake angelia. Mt. Allamano angesema baadaye: "Inaonekana kana mwamba haiwezekani: mama alikuwa na macho mawili kutoka peponi, na bado alikuwa kipofu". Alikufa mnamo 1870, wakati Mt. Allamano alikuwa na umri wa miaka 19. Alikuwa katika seminari na yule aliyetakiwa kumpa barua hiyo, aliisahau mfukoni. Aliteseka sana, lakini baba wake wa kiroho alimshauri kutoa dasaka hiyo na maumivu kwa Bwana, akimhakikishia kwamba Bwana angechukua mahali pa wazazi wake. Hiyo ilikuwa kwake fursa ya kuzungumza juu ya kutengana na wazazi ...

Baba yetu ....
Salamu Maria...


**SOMO: Luka 2:41-52** **(Wazo kuu: Mama na Baba Mlezi wa Yesu wahangaikia mtoto wao)**

*(Baada ya tafakari fupi)*
Atukuzwe Baba na Mwana...

**Kiongozi:**

**SALA:** Mt. Joseph Allamano, ulipitia matunzo na upendo wa mama. Ulimpenda na ulipitia upendo wake kwako, kwa familia yako na kwa wale wanaohitaji. Utuombee tumshukuru Mungu kwa ajili ya mama zetu. Wabariki na utuwezeshe kuwatunza maisha yao yote. Waombee akina mama wote ili waweze kuweka ndani ya watoto wao tunu za maisha ya Kikristo. Mama yetu Maria aombee akina mama wote na sisi sote. Maria Consolata, utuombee! Mtakatifu Joseph, mfanyakazi utuombee! Mt. Joseph Allamano, utuombee!

## Siku ya 3 - Allamano na ndugu zake



**Kwa jina la Baba...**
**Wimbo wa Mt. Allamano**

Mt. Joseph Allamano alikuwa na kaka wengine watatu na dada mmoja. Alikuwa na ukaribu fulani wa kipekee na Ottavio, kaka mdogo, tangu umri wao mdogo. Walikuwa wakiwasiliana wao kwa wao mara nyingi. Mt. Allamano alimjulisha yote yaliyokuwa yakitokea, majukumu aliyokuwa amekabidhiwa, n.k.

Mnamo 1868, kaka yake alipata ajali ambayo ilisababisha kukatwa mkono wake. Alipokuwa akipiga kengele Kanisani, alivunja mkono wake. Daktari aliufunga kwa nguvu sana hivi kwamba damu haingeweza kuzunguka. Baada ya madaktari wengine wengi kumuona waliamua kuukata mkono. Ilikuwa ni operesheni ya saa moja na bila anesthesia. Mwenye heri Allamano anatuandikia: “Fikiria uchungu wa mama yangu, dada yangu, kaka zangu na mimi mwenyewe. Ulikuwa wakati mgumu sana. Mkono wa Mungu ulikuwa umetuangukia sana… Ni muujiza wa Mungu kwamba alivumilia operesheni hiyo. Alikuwa na maumivu makali zaidi, na bado alibaki na ufahamu kote. Ahimidiwe Mungu aliyemsaidia baada ya upasuaji na kumsaidia kupona kwa haraka”.

Kuna barua nzuri kutoka kwa Ottavio iliyoandikwa kwa Mt. Allamano siku ya Mt. Joseph mnamo 1879:

Ndugu yangu mpendwa, katika siku hii adhimu, sikukuu yako, napaswa kukueleza hisia kutoka moyoni mwangu ili kuweka msingi wa uhusiano wa damu na urafiki ambao unapaswa kutuunganisha daima. Ninapaswa kulitaja jina lake ambaye alikuwa mwanzilishi wa kuwepo kwetu na ambaye hatukupata muda mwingi wa kueleza kwake ukiri wetu; jina la mama yetu mpendwa ambaye alitakaswa kwa matendo yake na hasa kwa ushuhuda wake ya muda mrefu; na



**SOMO:Luka 6:13-16 (Wazo kuu: Kama mitume, tunaitwa ili tuwe chachu ya mabadiliko duniani.**

*(Baada ya tafakari fupi)*
Atukuzwe Baba na Mwana...

**SALA**: Mt. Joseph Allamano, tunakushukuru kwa kuunda shirika la Wamisionari wa Consolata, Mapadre na mabruda, wanaojitolea kutangaza Habari Njema kwa Ulimwengu. Uwaombee ili waendelee kuwa waaminifu kwa wito wao, lakini zaidi ya yote, uwaombee ili wawe daima moyo mmoja na roho mmoja, wakisaidiana na kuheshimiana, kwa utajiri wao na tofauti zao. Utuombee sisi sote, ikiwa ni pamoja na walei, ili tuweze kuunda familia kubwa ya kimisionari, sio tu kujitegemeza wenyewe, bali kujitolea kwa Uinjilishaji wa Watu. Maria Consolata, utuombee! Mtakatifu Joseph, mfanyakazi utuombee! Mt. Joseph Allamano, utuombee!



## Siku ya 7 - Allamano na Wamisionari wa Consolata



**Kwa jina la Baba...**
**Wimbo wa Mt. Allamano**

Mwaka 1901 baada ya mchakato mrefu wa ndoto, sala, tafakari na zaidi ya yote uponyaji wa kimiujiza na Mama yetu Consolata, Mt. Joseph Allamano alianzisha Wamisionari wa Consolata, ili kukamilisha kazi iliyoanza na kusimamiwa na Kardinali Massaia nchini Ethiopia.

Hata hivyo, haikuwa tu kuhusu kuanzisha jumuiya ya wamisionari. Ilikuwa ni kuhusu kuunda Familia ya Wamisionari ambapo washiriki wangeweza kuja pamoja na kusaidiana katika kuweka maisha yao wakfu kwa misioni. Aliwaambia wamisionari wachanga katika matukio tofauti: Sitaki hii iwe seminari bali familia. Usiishi hapa kama wale wanaokuja bila kujuana, wanaishi kana kwamba hawapendani na mwishoni wanakufa bila kuliliana!

Wakati fulani aliwaandikia wamisionari wake nchini Kenya: "Sifa nyingine muhimu katika kazi ya umisionari ni ile ya umoja. Umoja wa akili na moyo hurahisisha kazi na magumu, hutia watu nguvu na kuwapatia ushindi... Fanyeni kazi pamoja kwa upatanifu, na Mungu atabariki juhudi na kazi zenu za pamoja."

Mt. Allamano alianzisha Wamisionari wa Consolata ili hata wakati wamisionari kutokana na changamoto za afya zao na matatizo mengine, wanashindwa kuishi tena katika umisheni, waweze kurejea katika jumuiya yoyote ile na kupata bado familia inayowakaribisha.

Baba yetu ....
Salamu Maria...



jina la mjomba wangu ambaye tulifurahi sana kumsalimia wakati wa ujana wetu. Lakini nataka kutumia tukio hili sio tu kukutakia afya njema na furaha katika roho yako, lakini kukuuliza usali na uweke imani yako katika kuniombea mimi na familia yangu.

Nikifundishwa na uzoefu wa maisha yangu ya kawaida na kufahamu wajibu wangu wa juu ulio juu yangu, ninahisi haja ya kurejesha nguvu zangu dhaifu kwa nguvu ambayo haina asili ipasavyo; lakini natamani uniombee kwa Mkuu wa familia ya Nazareti (Mt. Joseph) ili nijue fadhila zinazofaa kuiongoza vizuri ile mashua, ambayo niliitwa kama rubani. Tafadhali simamia kupata kwa ajili yangu kwamba huyu Mtakatifu Mkuu ametia moyo ndani yangu na katika familia yangu ufahamu wa wajibu wetu na kwamba tuweze kuhimili wakati wa dhoruba za bahari hii. Haya ni matakwa kutoka kwa kaka yako Ottavio kwa niaba ya mke wake na ya malaika wetu mdogo.

Ottavio alioa mwaka 1877; alimaliza masomo yake mnamo 1878 na akafa mnamo 1879.

Baba yetu ....
Salamu Maria...

**SOMO: Marko 6:1-6** **(Wazo kuu: Ndugu wa Yesu – Tuwathamini ndugu zetu)**

*(Baada ya tafakari fupi)*
Atukuzwe Baba na Mwana...

**Kiongozi:**

**SALA:** Mt. Joseph Allamano, tunawasilisha kweko ndugu na dada zetu. Utuombee ili tuwatambue daima na kuweza kuwasaidia kwa njia yoyote ile tunayoweza. Uwaombee wao na familia zao katika mahitaji yao mbalimbali, lakini zaidi ya yote ili waweze kumjua Mungu na kumtumikia kwa moyo safi. Maria Consolata, utuombee! Mtakatifu Joseph, mfanyakazi utuombee! Mt. Joseph Allamano, utuombee!

## Siku ya 4 - Allamano na wajomba zake, Fr. John Allamano na Mtakatifu Joseph Cafasso



**Kwa jina la Baba...**
**Wimbo wa Mt. Allamano**

Fr. John Allamano alikuwa kaka wa baba yake Mt. Joseph Allamano. Alikuwa paroko katika kijiji kidogo (Passerano) na alitunza watoto wadogo baada ya kifo cha baba zao. Ni yeye aliishia kumwongoza Mt. Allamano katika kuacha shule ya Don Bosco ili kupata mwelekeo na wito wake.

Badala yake, Mtakatifu Joseph Cafasso alikuwa kaka yake Marianna Cafasso, mama yake Mt. Joseph Allamano. Walikuwa karibu sana hata kama alikutana naye mara moja tu, alipokuwa na umri wa miaka 6. Tukio hilo lilibaki akilini mwake milele. Hata hivyo aliweza kusikia mengi kumhusu. Hiyo inaeleza maana kwa juhudi ambazo Mt. Allamano aliweka katika kufanyia kazi kwa ajili ya Kutawazwa kwa mjomba wake mkubwa, jambo ambalo alifanikiwa kufanikiwa na kuwepo Roma kwa tukio hilo.

Kwa hakika, mwaka wa 1825, yaani miaka 70 baadaye, alipokwenda Castelnuovo kwa ajili ya sikukuu ya kutangazwa kwa Cafasso kuwa mwenye heri, Mt. Allamano alifaulu kubainisha mahali ambapo alikutana na mjomba wake ambaye aliweka mkono wake kichwani, na kusema “Na hapa ndipo nilipopata baraka zake”. Tukio ambalo, hata kama si kubwa, lilikuwa limevutia akili yake.

Mt. Allamano anapoandika katika mchakato wa Kutawazwa kwa Cafasso mjomba wake kuwa mwenye heri, anaandika: “Tangu nilipokuwa mdogo, nilisikia watu nyumbani na wengine kutoka kijijini wakiongea vizuri kuhusu mtumishi wa Mungu Cafasso, kana kwamba walikuwa wakizungumzia kuhusu kuhani wa kielelezo, aliyejaa upendo. Nilikuja kumvutiwa naye; Huo mvuto ulikua nikiwa katika shule ya Don Bosco.



alitaka kuzungumza lakini hakuweza. Aliangalia mbinguni na kusema tu ... "Mapenzi ya Mungu"

Ulikuwa ni urafiki wenye msingi wa kuthaminiana, kuheshimu vipaji vya kila mmoja. Joseph Allamano alikuwa daima mkuu; James Camisassa alikuwa daima wa pili, mtekelezaji mwaminifu na mwenye akili wa miradi yote.


Baba yetu ....
Salamu Maria...

**SOMO: Yohane 15:10-17** **(Wazo kuu: Urafiki wa kweli ni urafiki wa kimungu)**

*(Baada ya tafakari fupi)*
Atukuzwe Baba na Mwana...

**SALA**: Mt. Joseph Allamano, ulijua maana ya kuwa na rafiki mzuri karibu nawe. Ukiwa mwingi wa heshima kwa mwenzako, ulitengeneza uwezo unaoheshimika na kuunganisha pamoja katika mradi mmoja na upendo mmoja: Mungu na Utume. Utuombee ili tuweze kutengeneza na kushirikiana ili kuzalisha urafiki ambao unampa Mungu utukufu na kazi yake, badala ya kutafuta faida za binafsi. Maria Consolata, utuombee! Mtakatifu Joseph, mfanyakazi utuombee! Mt. Joseph Allamano, utuombee!

## Siku ya 6 - Allamano na Fr James Camisassa




**Kwa jina la Baba...**
**Wimbo wa Mt. Allamano**

Mara nyingi, Mt. Allamano alipopewa jukumu, aliuliza fursa ya kuchagua washiriki wake. Mara moja, alipoteuliwa kuwa mkurugenzi wa kanisa la hija la Consolata huko Torino, alimwita padre James Camisassa kuwa msaidizi wake kwa miaka 42 iliyobaki ya maisha yake. Hakuwa msaidizi tu, bali pia rafiki na ndugu. Kuanzia wakati huo na kuendelea maisha ya Allamano yaliwekwa alama sana na mtu huyu, ambaye aliweza kubaki katika nafasi ya pili katika maisha na kazi zao.

Padre Camisassa hakuwa ametoa tu talanta zake na ujuzi wake, lakini zaidi ya yote alijitolea mwenyewe kwa Joseph Allamano kufanya kazi kwa ajili ya Misioni na Wamisionari. Akawa Makamu Mkuu wa Shrine ya Consolata na kuchukua jukumu muhimu sana pia katika kuazishwa kwa Masista Wamisionari wa Consolata.

Padre Domenico Ferrero alipokwenda kumtembelea Joseph Allamano kwenye shrine ya Consolata huko Torino, na akijua jinsi Padre Camisassa alikuwa mgonjwa, alimwambia Joseph Allamano: “Baba, unaweza kumtolea Mungu uhai wa yeyote kati yetu kama kubadilishana maisha ya Makamu Mkuu!” Mt. Allamano alijibu: "Tayari nimetoa uhai wangu, lakini inaonekana hauna maana!" na akakaa kimya.

Wakati Mt. Allamano alitoka kwenye chumba ulipokuwa umewekwa mwili wa James Camisassa, alionekana kuwa "sanamu ya maumivu",



Na baadaye kupitia mawasiliano na makasisi wa jimbo, nilikuja kumpenda zaidi na zaidi…”

Mt. Allamano alijua kwamba hapakuwa na kitu cha ajabu katika Cafasso: alikuwa kuhani aliyetenda kila kitu kwa njia ya "ajabu katika kawaida", ambaye mara nyingi alikuwa akisema "mema lazima yafanywe vizuri". Alihangaikia kutangazwa kwa Joseph Cafasso kuwa mwenyeheri, sio kwa sababu walikuwa watu wa ukoo mmoja, bali kama yeye mwenyewe alivyosema akizungumza wakati mmoja na wamisionari: “Kwa ajili ya wema ambao kuinuliwa kwake mtu huyu kungeweza kufanya. Ili wale wote ambao wangesoma juu ya fadhila zake wawe makuhani wazuri, Wakristo wazuri na ninyi… wamisionari wazuri”.

Mt. Allamano na Joseph Cafasso pia walifanana sana. Kwa hakika, mmoja yeyote alipotaka kuchora picha ya Joseph Cafasso, alimuomba Joseph Allamano aketi ili kumchora yeye.

Baba yetu ....
Salamu Maria...

**SOMO: Mathayo 12:46-50** **(Wazo kuu: jamaa za Yesu -> Neno la Mungu latufanya sehemu ya familia ya Yesu).**

*(Baada ya tafakari fupi)*
Atukuzwe Baba na Mwana...

**Kiongozi:**

**SALA**: Mt. Joseph Allamano, ulioja mapenzi ya mjomba wako, hasa pale ulipomkosa baba yako mzazi. Pia ulipokea baraka za mjomba wako Mtakatifu Joseph Cafasso, ambaye kutoka kwake ulitambua fadhila na utakatifu. Tuombee ili tuweze kutambua thamani ya jamaa zetu katika familia zetu na kujifunza kutoka kwao. Waombee jamaa zetu ili wafahamu jinsi wanavyoweza kuwa msaada kwetu, hasa katika kutulea katika maadili ya kibinadamu na ya Kikristo zaidi ya yote. Maria Consolata, utuombee! Mtakatifu Joseph, mfanyakazi utuombee! Mt. Joseph Allamano, utuombee!

## Siku ya 5 - Allamano na mwalimu wake, Benedetta Savio



**Kwa jina la Baba...**
**Wimbo wa Mt. Allamano**

Akiwa Castelnuovo, Joseph Allamano alihudhuria chekechea ambayo Benedetta Savio alikuwa ndiye mkurugenzi. Mara moja, uhusiano mpya ulizaliwa kati ya mkurugenzi na mwanafunzi wake mdogo.

Mt. Allamano, akifahamu mema yote aliyopokea kutoka kwake, hakumsahau kamwe. Alikuwa na heshima kubwa sana kwamba alipokufa, alitafuta mtu kuandika kuhusu maisha yake. Vivyo hivyo, hata Benedetta Savio hakuweza kumsahau Allamano, kwa hivyo waliendelea kuandikiana, kutembeleana, kukusanya habari kuhusu Joseph Cafasso, nk. Pia waliandikiana sana wakati mmoja wa jamaa zao aliaga, ili kufarijiana.

Alipokufa Benedetta mwaka wa 1896, Joseph Allamano alimwandikia kasisi, ambaye alikuwa mpwa wake: "Mwalimu wetu mwema amepaa kuingia Paradiso; Bwana alimtakasa kwa misalaba ya mwaka huu, kufikia sasa anaweza kuwa tayari amekutana na Don Cafasso".

Baba yetu ....
Salamu Maria...

**SOMO: Waefeso 4:11-16** **(Wazo kuu: Ualimu ni kipaji cha Mungu. Tuwasikilize kwa makini, tuwaheshimu, na kuwatia moyo).**



*(Baada ya tafakari fupi)*
Atukuzwe Baba na Mwana...

**Kiongozi:**

**SALA**: Mt. Joseph Allamano, ulikuwa na heshima na upendo wa hali ya juu kwa wale waliokufundisha. Uliona wazi ndani yao kazi ya Mungu. Utuombee ili kutambua kazi ya wale wote waliotufundisha sisi na wale wote wenye mamlaka, ili tuweze kutunza mawasiliano nao na kuwaonyesha shukrani zetu. Waombee ili yeyote anayechukua jukumu la kuwa mwalimu au kiongozi, asisahau kamwe kwamba wameitwa kuwa chombo cha Mungu. Maria Consolata, utuombee! Mtakatifu Joseph, mfanyakazi utuombee! Mt. Joseph Allamano, utuombee!

